

MAELEZO MUHIMU KATIKA KUFUNGUA JALADA (FILE) LA MIRATHI

Ili uweze kufungua jalada la mirathi na kupata haki yako ya mirathi unapaswa kufuata hatua zifuatazo:-

1. UNATAKIWA KUFANYA MALIPO YA FOMU YA KUFUNGULIA TIRKA

Mwanachi (Mteja) atapewa namba ya Akaunti na atakwenda kulipa **TZS. 2,000/-** katika Tawi lolote la Benki ya Watu wa Zanzibar (**PBZ YA KAWAIDA NA SIO ISLAMIC**). Baada ya hapo anatakiwa kuwasilisha Slip ya Benki Ofisini (**KIDIRISHA NAM. 6**) atapewa risiti yake na atakabidhiwa **FOMU YA KUFUNGUA TIRKA**. Fomu hiyo itajazwa na Sheha wa Shehia aliyokuwa anaishi marehemu au Shehia iliyopo mali kwa mali isiyohamishika.

2. VITU (VIELELEZO) VINAVYOTAKIWA KUWEMO NDANI YA JALADA (FILE)

Baada ya Sheha kuijaza fomu, mteja atairejesha fomu ofisini pamoja na vitu vifuatavyo:-

a). Kopi ya cheti cha kifo cha mwenye mali.

b). Kopi ya vitambulisho vyenye picha vya warithi wote, ikiwa hana kitambulisho alete kopi ya cheti cha kuzaliwa au barua ya Sheha yenye picha ya mrithi itakayomthibisha kuwa ni mrithi.

c). Bank statement/ Slip au kadi ya benki ikiwa marehemu ameacha fedha benki.

d). Waraka wa nyumba/shamba pamoja na picha zake na ikiwa hakuna waraka utaleta barua ya Sheha inayothibitisha umiliki wa nyumba au shamba pamoja na mipaka yake na kiapo cha Mahakama Kuu.

e). Ikiwa marehemu ana mrithi mmoja (**Mrithi pekee**) atalazimika kuleta kiapo cha Mahakama Kuu kitakachothibitisha kuwa yeye ni mrithi pekee na atatoa tangazo katika gazeti ili kama kuna pingamizi yoyote dhidi yake iweze kufikishwa Kamisheni ya Wakfu ndani ya siku 14.

3. MAELEZO YA WARITHI

Warithi wote watakaokuwa na umri usiopungua miaka 18 wanatakiwa kufika Ofisini na kutoa maelezo yao juu ya mali, madeni, wasia na warithi aliowaacha Marehemu. Endapo kutakuwa na dharura isiyoepukika wanaweza kutoa maelezo baadhi ya warithi au wanaweza kutengeneza Hati ya Uwakala.

**IMEANDALIWA NA KITENGO CHA URITHI, KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA -
ZANZIBAR**